



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS



TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Mtaa wa Utumishi 10 Mtumba, S.L.P. 1074, 41207 DODOMA. Nambari ya simu: 026-2610780,
Barua pepe: secretary@psc.go.tz, Tovuti: www.psc.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

Tume ya Utumishi wa Umma ni Chombo Rekebu kilichoanzishwa chini ya Kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, sura ya 298 (Marejeo ya mwaka 2023) chenye wajibu wa kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo.

Mkutano wa kwanza wa Tume ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ulifanyika chini ya Mwenyekiti wake **Jaji (Mst.) Hamisa H. Kalombola**, kuanzia tarehe 21/09/2026 hadi tarehe 16/10/2026, katika Ukumbi wa mikutano wa Ofisi za Tume ya Utumishi wa Umma zilizopo Mji wa Serikali Mtumba, Jijini Dodoma.

Katika Mkutano huu, Tume ilijadili na kutoa uamuzi wa Rufaa na Malalamiko mbali mbali yaliyowasilishwa na Watumishi wa Umma ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka zao za Nidhamu katika Utumishi wa Umma.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 12(1)(d) na Kifungu 27(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 (Marejeo ya mwaka 2023), Tume ilitolea uamuzi Rufaa na Malalamiko **74** yaliyowasilishwa mbele yake ambapo rufaa zilikuwa **57** na Malalamiko **17**.

Katika Rufaa zilizowasilishwa na kuamuliwa na Tume, makosa yaliyoonekana kutendwa zaidi na Watumishi wa Umma ni pamoja na:-

- (i) Utoro kazini;
- (ii) Kushindwa kutekeleza majukumu;
- (iii) Wizi wa mali za Umma na rushwa;
- (iv) Kughushi vyeti;
- (v) Kutoa taarifa za uongo;

Kwa upande wa Malalamiko, yaliyowasilishwa na kuamuliwa na Tume yalihusu kupinga mambo yafuatayo:-

- (i) Kutenguliwa katika cheo;
- (ii) Kutorudishwa kazini;
- (iii) Kusitishiwa ajira;
- (iv) Kuondolewa kwenye Orodha ya Mishahara.
- (v) Kutopandishwa cheo;

Katika Mkutano huu, jumla ya Warufani **18** na Mrufaniwa **mmoja (1)**, walifika mbele ya Tume kusikilizwa. Aidha, Mamlaka za Nidhamu **mbili (2)** ziliitwa na kufika mbele ya Tume kuhojiwa kutokana na ukiukwaji wa Sheria zilizofanya katika kushughulikia mashauri ya Nidhamu ya Watumishi walio chini yao.

Aidha, Tume katika kipindi hiki cha Mkutano, Tume ilifanya ziara katika Taasisi 14 za Serikali zilizopo Mkoani Dodoma, kwa lengo la kutoa elimu juu

ya masuala mbali mbali ya Utumishi wa Umma. Lengo kuu la ziara hizi ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Urekebu, ambapo Utumishi wa Umma unapaswa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Hii imetokana na changamoto nyingi zinazojitokeza katika usimamizi wa Utumishi wa Umma ikiwemo masuala ya kutofuata utaratibu, kutozingatia maelekezo ya Serikali na wakati mwingine ufahamu mdogo wa masuala ya Kiutumishi.

Tume pia, ilipata fursa ya kupokea na kupitia Taarifa za Utelezaji wa Majukumu ya Tume **saba (7)** na kuzitolea maelekezo kabla ya kuwasilishwa kwenye mamlaka mbalimbali za Serikali.

Tume inaendelea kuwakumbusha Watumishi wa Umma kuzingatia Sheria ili kujiepusha na Vitendo vinavyoashiria ukiukwaji wa Maadili, hali inayoweza kusababisha kuchukuliwa hatua za Kinidhamu au za Kijinai.

Ni muhimu kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu kuendelea kuzingatia Sheria wakati wa kushughulikia Malalamiko na Mashauri ya Nidhamu ya Watumishi ili haki si tu itendeke bali ionekane inatendeka.

IMETOLEWA NA:-



Nolasco J. Kipanda

KATIBU

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

22/10/2026